

Hujambo St. Louis!

Je, unajaribu kupata chanjo ya COVID-19?

Hii ni fursa nyingine!

Ugavi wa chanjo ya COVID-19 umeongezeka hapa Missouri. Wakazi wa St. Louis sasa wana njia nyingine ya kupata chanjo ya COVID-19 kwa kufunguliwa kwa Kituo cha Chanjo ya Jamii (CVC) katikati mwa jiji.

Ili kupata miadi, unahitaji kujiandikisha kwenye tovuti ya chanjo ya Jimbo la Missouri. Ikiwa tayari umejiandikisha kwenye tovuti ya chanjo (kama Jiji la St. Louis, Kaunti ya St. Louis au nyingine) **LAZIMA ujisajili tena kwenye tovuti ya jimbo.**

Hii hapa ni njia ya kujiandikisha:

Kwenye mtandao: Tovuti ya Chanjo ya Missouri:

<https://covidvaccine.mo.gov/navigator/>



Au piga simu: (877) 435-8411

Kituo cha Chanjo ya Jamii

Lini: Aprili 7 - Juni 1

Wapi: The Dome at America's Center

Masaa: Saa mbili asubuhi (8 a.m.) hadi saa kumi na mbili jioni (6 p.m.), siku 7 kwa wiki (mpaka mtakapojulishwa tena)



FEMA